

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI  
MTIHANI WA PAMOJA KIDATO CHA PILI 2021

MUDA:

SEHEMU A (ALAMA 15)

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yafuatayo

Hali iliyopo kwenye shule zetu hivi sasa inaelewwka. Watoto wanalazimika kusoma katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukaa chini, kusoma bila vifaa muhimu na kurundikana katika chumba kimoja cha darasa.

Vilevile walimu pia wanakabiliana na hali ngumu ya maisha inatokana na kipato duni, ukosefu wa nyumba, uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi na ucheleweshaji wa mishaharayo.

Matatizo hayo yote kwa hakika, yanawaathiri sana walimu kiutendaji na kuifanya kazi ya kusimamia nidhamu ya wanafunzi kuwa ngumu sana. Katika mazingira haya ya kazi wengi huttumia viboko kama njia rahisi ya kurekebisha tabia ya wanafunzi.

Hata hivyo kutumia nguvu au kupiga bado sio ufumbuzi wa kuisha kwa matatizo ya kiinidhamu shuleni. Pale inapobidi walimu kuadhibu basi wanashauriwa kutoa adhabu ambazo zitamsaidia mwanafunzi kuelwa kosa lake na kujirekebisha.

Maswali

- a) Andika kichwa cha habari uliyosoma kwa maneno yasiozidi matano
  - b) Taja matatizo matatu yanayokabili walimu
  - c) Kwa nini adhabu ya viboko haifai kurekebisha tabia za wanafunzi?
  - d) Taja matatizo mawili yanakabiri wanafunzi
  - e) Walimu wanashauriwa nini inapowalazimu kutoa adhabu?
2. Andika ufupisho wa habari uliyosoma kwa maneno sitini (60)

SEHEMU B (ALAMA 20)

3. (a) taja kauli zilizotumika kuunda maneno yafuatayo

- i. Umekatika
- ii. Nimemchezesha
- iii. Wanaandikiana
- iv. Amepigwa
- v. Anatetemeka

(b) Nyumbua maneno yafuatayo na kuunda maneno matatu kwa kila neno

- i. Angalia
- ii. Chukua
- iii. Oga
- iv. Kata
- v. Omba

4. Sentensi zifuatazo zimetumia njeo tofauti tofauti. Taja njeo hizo kwa kila sentensi moja
- a) Tutawaona wakija polepole
  - b) Wanatembea haraka haraka
  - c) Aliona gari likipinduka
  - d) Motto hakusoma kitabu
  - e) Mtoto akilala tutaondoka
  - f) Mwalimu anafundisha darasani
  - g) Baba hulima shamba
  - h) Juma angekuja tungeondoka
  - i) Mnvua imenysha usiku
  - j) Mimea hii inanyauka

SEHEMU C (ALAMA 20)

5. Elezea maanaya istilahi zifuatazo, Toa mfano kwa kila maana ya istilahi
- a) Mnyambuliko
    - i. Maana
    - ii. Mfano
  - b) Sarufi
    - i. Maana
    - ii. Mfano
  - c) Utata
    - i. Maana
    - ii. Mfano
  - d) Mofimu
    - i. Maana
    - ii. Mfano
  - e) Mzizi wa neno
    - i. Maana
    - ii. Mfano
6. (a) Taja miktadha ambamo maneno yafuatayo hutumika
- i. Nani chai?
  - ii. Baba yesu, niokoe
  - iii. Mchele kilo mbili tu
  - iv. Chapa hizi barua
  - v. Baharia, nahodha, natia

(b) Toa tofauti tano (05) kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi

SEHEMU D (ALAMA 30)

FASIHI KWA UJUMLA

7. Kamilisha methali zifuatazo
  - i. Aliye juu
  - ii. Bora lawama
  - iii. Chelewa chelewa
  - iv. Ganda la mua la jana
  - v. Maneno matamu
8. Taja njia tano (05) zinazotumika kuhifadhia kazi ya fasihi simulizi
9. Taja vipengele vitano (05) vinavyounda fani na maudhui

SEHEMU E (ALAMA 15)

UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI

10. Unatarajia kwenda kuanza kambi shuleni kwako kwa ajili ya kujiandaa na mitihani wa mwisho wa kidato cha pili. Mwandikie barua baba yako kumwomba mahitaji ya lazima ili kutimiza lengo lako. Jina lako liwe Jembe Mpini, Shule ya Mapambano, S. L. P 1534, mchangani, Mara.